

KUZUIA SURUA

KABLA NA BAADA YA KUSAFIRI



Surua inaweza kuwa hatari, hasa kwa watoto wachanga na wadogo. Surua kali inaweza kupelekea kulazwa hospitalini na hata kifo.

Surua bado ni ya kawaida katika maeneo mengi duniani. Mtu yeyote ambaye hajapewa chanjo kamili dhidi ya surua na anasafiri kimataifa au kwenda eneo lenye mlipuko wa surua yupo hatarini.



Unaweza kujilinda wewe na watoto wako dhidi ya surua kwa kupata chanjo ya surua, matumbwitumbwi, na rubela (MMR).

Cha kufanya KABLA ya kusafiri kimataifa

1. Zungumza na daktari wako, muuguzi, au kliniki ili kuhakikisha kila mtu amelindwa dhidi ya surua.
2. Pata chanjo hiyo angalau wiki 2 kabla ya kusafiri.
 - Watoto wachanga wenye umri wa miezi 6 hadi 11 wanapaswa kupata dozi moja ya chanjo ya MMR.
 - Kila mtu mwenye umri wa miezi 12 na zaidi (ikiwa ni pamoja na watu wazima) anatakiwa kupata jumla ya dozi 2 kabla ya kusafiri.
 - Ikiwa hujapata chanjo hapo awali, pata dozi ya kwanza mara moja. Unaweza kupata dozi ya pili baada ya siku 28.
 - Ikiwa tayari umepata dozi moja, pata dozi ya pili kabla ya kusafiri.
3. Hata kama safari yako imebaki chini ya wiki 2, bado unaweza kupata dozi moja ya chanjo ya MMR.

Ikiwa unapanga kusafiri kwenda eneo la Marekani lenye mlipuko wa surua, zungumza na daktari wako, muuguzi, au kliniki ili kuhakikisha kila mtu amelindwa dhidi ya surua.



Cha kufanya BAADA ya kusafiri kimataifa au kwenda eneo lenye mlipuko wa surua

1. Angalia dalili za surua kwa muda wa wiki 3 baada ya kurudi. Surua **inaambukiza sana** na inaweza kuenea kwa wengine haraka.
2. Piga simu kwa daktari au kliniki MARA MOJA ikiwa:
 - Unadhani wewe au mtoto wako mmeambukizwa surua.
 - Wewe au mtoto wako anaumwa na ana vipele pamoja na homa. Mwambie daktari wako uliposafiri, na ikiwa wewe na mtoto wako mmepeleka chanjo ya MMR.
3. Ikiwa wewe au mtoto wako anaumwa na ana vipele pamoja na homa, baki nyumbani hadi uongee na daktari au kliniki.